
# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA AFYA

## MPANGO WA TAIFA WA KIFUA KIKUU NA UKOMA



# MKATABA WA HUDUMA KWA WAGONJWA WA KIFUA KIKUU TANZANIA

JUNI 2021

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA AFYA

## MPANGO WA TAIFA WA KIFUA KIKUU NA UKOMA

# MKATABA WA HUDUMA KWA WAGONJWA WA KIFUA KIKUU TANZANIA

JUNI 2021

## MKATABA WA HUDUMA KWA WATEJA WA KLINIKI ZA KIFUA KIKUU

## 1. HAKI ZA MGONJWA WA KIFUA KIKUU

Mhisiwa au mgonjwa wa Kifua Kikuu ana haki zifuatazo:-

### 1.1 Haki ya Kupata Huduma:

**Mteja ana haki ya;**

1.1.1 Kupata huduma kwa wakati bila malipo, bila kukatishwa wala ubaguzi wa aina yoyote;




1.1.2 Kupata ushauri wa kitabibu unaokidhi viwango vya kitaifa vya matibabu ya kifua kikuu ikiwemo ushauri kuhusina na maudhi ya dawa;



1.1.3 Kupata huduma zinazokidhi mahitaji ya makundi maalum kama vile wenye kifua kikuu sugu, maambukizi mseto ya kifua kikuu na UKIMWI na kutoa kinga kwa watoto na makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kupata maambukizi;



1.1.4 Kupata chakula dawa  wakati wa matibabu kwa wagonjwa wenye utapia mlo;





1.1.5 Kupata huduma za dharura kwa wagonjwa kama vile wanao pumua kwa shida, kubanwa na kifua, na wanaopata maudhi makubwa ya dawa.

## 1.2 Haki ya utu na heshima

Mteja ana haki zifuatazo:

1.2.1 Mteja, familia na wanaomhudumia mgonjwa wana haki ya kuhudumiwa kwa kuzingatia utu, heshima, upendo na huruma;



1.2.2 Kutonyanyapaliwa wala kubaguliwa;

1.2.3 Kupata huduma bora katika mazingira yanayozingatia utu na heshima, kusikilizwa maoni yake na matatizo yake;



1.2.4 Kupewa heshima na kufuata imani za kidini na za kiutamaduni bila ya kunyanyaswa ili mradi Imani hizo haziathiri taratibu za matibabu; na

1.2.5 kuitwa kwa jina lake na siyo kwa tatizo alilonalo, rangi, ulemavu, umri, kabila au utaifa.

## 1.3 Haki ya kupata taarifa;-

Mteja ana haki ya kupata taarifa kuhusiana na;

1.3.1 Huduma za kifua kikuu zilizopo, wajibu, ushiriki wa mgonjwa pamoja na malipo ya ziada endapo yatahitajika;

1.3.2 Majibu ya vipimo vya awali, vipimo vingine vitakavyohitajika, muda wa matibabu na maendeleo ya matibabu yake;

1.3.3 Ugonjwa alionao, matokeo ya uchunguzi, aina ya matibabu, dawa na dozi atakayopewa, maelezo juu ya ufanyaji kazi wa dawa pamoja na madhara yanayoweza kutokea kwa kutumia dawa alizopewa;

1.3.4 Elimu ya afya na ushauri kuhusu kifua kikuu ikiwemo kinavyoam bukiza, uchunguzi, kinga na lishe;



1.3.5 Mwenendo, mabadiliko na matarajio ya matibabu;

1.3.6 Mbinu za kukabiliana na maudhi ya dawa endapo yatatokea pamoja na mabadiliko ya tiba itakapolazimu; na

1.3.7 Jina na cheo cha mtoa huduma anayemhudumia.

**1.4 Haki ya kuchagua**

Mteja ana haki ya kuchagua:

1.4.1 Kituo cha kupatia huduma;

1.4.2 Kumezea dawa kituoni au nyumbani;

1.4.3 Msimamizi wa matibabu endapo atamezea nyumbani;

1.4.4 Kushiriki au kutokushiriki katika tafiti mbalimbali zinazohusu ugonjwa wa kifua kikuu bila kuathiri matibabu yake;

1.4.5 Kupata maoni ya kitalaam kutoka kwa watalaam wengine; na

1.4.6 Kukubali au kukataa upasuaji endapo ugonjwa unaweza kutibika kwa njia nyingine

**1.5 Usiri na faragha**

**Mteja ana haki ya;**

1.5.1 Kupata faragha wakati wa matibabu;

1.5.2 Kutunziwa taarifa za matibabu kwa usiri wakati wa matibabu na baada ya kufariki isipokuwa kwa kufuata taratibu zilizopo endapo taarifa zake zitahitajika;


1.5.3 Kuridhia taarifa zake kutolewa kwa mtu wa tatu kwa mujibu wa taratibu zilizopo; na

1.5.4 Kupewa kadi ya utambulisho wa ugonjwa kwa mgonjwa mwenyewe au msimamizi.

**1.6 Haki ya Malalamiko au Maoni.**

Mteja ana haki ya;

1.6.1 Kutoa maoni au malalamiko kuhusu huduma alizopata kupitia mifumo iliyowekwa na mamlaka husika kwa lengo la kuboresha huduma;



1.6.2 Kupata mrejesho wa maoni au malalamiko yaliyotolewa;

1.6.3 Kukata rufaa kwa mujibu wa taratibu zilizopo endapo hatua stahiki hazitachukuliwa kwa wakati.

**1.7 Haki ya Kujiunga na Asasi au kikundi**

Mteja ana haki ya kushiriki katika vikundi au Asasi ya watu wanaougua au waliougua na kupona kifua kikuu.

**1.8 Usalama wa Kazi**

Mteja ana haki ya kuendelea na kazi wakati na baada ya kumaliza matibabu ya kifua kikuu kwa kuzingatia miongozo iliyopo.

**1.9 Haki ya Usalama wa afya ya Mteja**

Mteja ana haki ya:-

1.9.1 Kupewa huduma na mtoa huduma anayetambuliwa na mamla ka husika;

1.9.2 kulindwa ili asipate maambukizi mapya wakati akiwa kwenye mazingira ya kutolea huduma za afya; na

1.9.3 Kupata huduma katika mazingira yenye nafasi, safi, uwazi na hewa ya kutosha.

**2. WAJIBU WA MGONJWA WA KIFUA KIKUU**

Mgonjwa wa Kifua kikuu ana wajibu wa kufanya yafuatayo:-

**2.1 Wajibu wa kutoa taarifa;**

2.1.1 Kutafuta matibabu mapema iwezekanavyo endapo mgonjwa ataona dalili mojawapo ya kifua kikuu ili watoa huduma waweze kutoa huduma stahiki kwa wakati;

2.1.2 Kuwapa watoa huduma za afya maelezo sahihi na ya kweli kuhusu maradhi yanayomsumbua na kikwazo chochote cha kutotumia aina fulani ya dawa ili waweze kutoa tiba kwa ufanisi;

2.1.3 Kutoa taarifa ya maendeleo ya afya yake na mabadiliko yoyote katika mwili au maudhi ya dawa wakati wa matibabu;

2.1.4 Kutoa taarifa pindi apatapo dharura yoyote itakayomfanya asiweze kuhudhuria kliniki kwa tarehe aliyopangiwa;

2.1.5 Kutoa taarifa kama kuna mtu mwingine mwenye dalili za ugonjwa wa kifua kikuu pale anapoishi;

2.1.6 Kutoa taarifa kama kuna watoto mahali anapoishi ikiwemo wale wenye umri chini ya miaka mitano; na

2.1.7 Kutoa maoni, malalamiko na mapendekezo kupitia njia sahihi za uwasilishaji zilizowekwa na kituo.

## 2.2 Wajibu wa Kufuatilia matibabu kwa ukamilifu

2.2.1 Kumeza dawa kwa usahihi kwa kuzingatia dozi na muda sahihi kwa kufuata maelekezo ya mtoa huduma wa afya;

2.2.2 Kushirikiana na msimamizi wa dawa wakati wote wa matibabu ili kuhakikisha dawa zinamezwa kwa usahihi kwa lengo la kulinda afya ya mgonjwa na ya jamii;

2.2.3 Kuzingatia tarehe ya kwenda kuchukua dawa na vipimo kama atakavyoshauriwa na watoa huduma wa afya;

2.2.4 Kuzingatia lishe bora pamoja na kutunza afya yako kwa kuzingatia mwenendo bora wa maisha ikiwemo kuzingatia miiko ya dawa kama kuepuka sigara na pombe;

2.2.5 Kutunza kumbukumbu za matibabu ulizonazo na kuzitoa wakati zinapohitajika na mtoa huduma za afya; na

2.2.6 Kufuata taratibu za uchangiaji wa matibabu na huduma za afya ikiwemo kujiunga na bima ya afya; na

2.2.7 Kumtaarifu mtoa huduma kama kuna tatizo lolote katika kufuatilia matibabu au kama kuna maelekezo ya matibabu ambayo hayajaeleweka.

## 2.3 Wajibu wa Kutoa mchango wa Afya kwa Jamii

2.3.1 Kuelimisha jamii inayomzunguka jinsi ya kujikinga na ugonjwa wa kifua kikuu;

2.3.2 Kumshauri mtu mwenye dalili za Kifua Kikuu kwenda kwenye kituo cha tiba kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi;

2.3.3 Kumshauri mtu aliyegundulika kuwa na kifua kikuu kufuata matibabu;

2.3.4 Kuhamasisha, kutoa ushauri na kuwatia moyo walioko kwenye matibabu;

2.3.5 Kutoa ushuhuda kuhusiana na uponaji wa ugonjwa wa kifua kikuu;

2.3.6 Kusisitiza ukohoaji salama kwa kufunika mdomo na pua wakati wa kukohoa na kutema mate au makohozi katika chombo chenye mfuniko ili kuzuia kusambaa kwa ugonjwa wa kifua kikuu; na

2.3.7 Kujali haki za wagonjwa wengine na watoa huduma za afya ili kutohatarisha afya na maisha yao.

2.4 Kuwa na mshikamano na wateja wengine, watoa huduma na jamii wakati na baada ya matibabu

2.4.1 Kushiriki katika shughuli za kuhamasisha jamiii kujikinga na kifua kikuu na kutafuta huduma za uchunguzi na tiba ya kifua kikuu;

2.4.2 Kuhimizana wenyewe kwa wenyewe kutumia dawa kwa usahihi;

2.4.3 Kutiana moyo na kubadilishana mawazo na uzoefu miongoni mwa wagonjwa ili kujengeana uwezo wa kudhibiti kifua kikuu ndani ya jamii;

2.4.4 Kushirikiana na wadau mbalimbali katika mapambano ya kudhibiti na kutokomeza Kifua Kikuu.

2.4.5 Kuwaheshimu na kuwajali watoa huduma ikiwa ni pamoja na kutumia lugha yenye staha;

2.4.6 Kulinda mali za kituo na kuweka mazingira ya kituo safi na salama; na

2.4.7 Kutokujihusisha na matendo yanayoweza kuhatarisha usalama wa wateja wengine na watoa huduma (mf: unywaji wa pombe au uvutaji/uingizaji dawa za kulevya/silaha ndani ya kituo cha kutolea huduma za afya.

**MSISITIZO!**
**ENDAPO MGONJWA WA KIFUA KIKUU ATAKATAA KUPATIWA MATIBABU AU KWENDA KULAZWA KWENYE HOSPITALI MAALUM ITAKAPOLAZIMU, ATACHUKULIWA HATUA KULINGANA NA SHERIA YA AFYA YA JAMII YA MWAKA 2009.**

amref health africa

Tanzania TB Community Network